# TAASISI YA MWALIMU NYERERE

**HOTUBA YA DR. SALIM AHMED SALIM, MWENYEKITI, TAASISI YA MWALIMU NYERERE**

**KWENYE UFUNGUZI WA KONGAMANO LA MAADHIMISHO YA MIAKA 10 YA MFUMO WA SIASA YA VYAMA VINGI TANZANIA, LILILOANDALIWA NA TAASISI YA BUNGE KWA AJILI YA DEMOKRASIA**

*Dar es Salaam,*
***2 Julai, 2002***

## HOTUBA YA DR. SALIM AHMED SALIM KWENYE UFUNGUZI WA KONGAMANO LA MAADHIMISHO YA MIAKA 10 YA MFUMO WA SIASA WA VYAMA VINGI TANZANIA

**Mheshimiwa Rais Mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi**

**Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilisha**

**Waheshimiwa Mawaziri**

**Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi**

**Viongozi wa Vyama vya Siasa**

**Washiriki wa Kongamano**

**Mabibi na Mabwana**

Naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu kwa Uongozi wa Taasisi ya Bunge kwa Ajili ya Demokrasia kwa kunialika kushiriki katika kongamano hili muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Ninawapongeza wote wanaohusika kwa kuandaa kongamano hili ambalo linatupatia fursa kutafakari kwa pamoja ujenzi wa taifa letu katika misingi inayokubalika ya demokrasia shirikishi ambayo hivi sasa imeanza kuchipua na kuota mizizi katika bara letu la Afrika.

Waheshimiwa washiriki wa kongamano hili; tunakutana leo kutafakari juu ya mfumo wa utawala na uongozi wa nchi yetu tangu tulipoamua miaka kumi iliyopita kuirejesha nchi yetu katika mfumo wa siasa wa demokrasia ya vyama vingi. Tunafanya hivyo ili kutafakari kwa undani tulikotoka, tulipofikia na namna ya kufika huko tuendako tukiwa bado taifa lenye mshikamano na umoja. Hili ni eneo ambalo Tanzania inayofursa nzuri ya kuendelea kuwa mfano kwa nchi nyingine za Afrika.

Suala la uimarishaji wa misingi ya utawala bora ni moja ya changamoto zinazotukabili viongozi wote wa Africa katika karne hii mpya. Misingi hiyo ya utawala bora ni pamoja na kujenga na kuimarisha mfumo wa siasa wa vyama vingi ambamo kila mdau anajihisi kuwa ana fursa na wajibu sawa na wadau wengine katika kuchangia jitihada za kuimarisha utawala bora. Na maana halisi ya utawala bora ni pamoja na kuwepo kwa demokrasia shirikishi. Watu wetu walishiriki katika harakati za kudai uhuru si tu kwa sababu waliona fedheha ya kutawaliwa na wageni ingawa hiyo ni sababu nzito. Lakini naamini pia waliingia harakati hizo ili wajirejeshee haki ya kujiamulia mambo yao wenyewe. Kwa hiyo kupatikana kwa uhuru hapa Tanzania Bara pamoja na Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ni mwanzo tu wa safari ndefu ya kuelekea kwenye demokrasi shirikishi.

Demokrasia si taasisi bali ni mfumo wa siasa unaowapatia fursa sawa wanajamii kutoa mawazo yao juu ya uendeshaji wa mambo yanayowahusu na kuamua hatma ya jamii yao kwa kutekeleza kila mmoja wajibu wake katika ujumla wake. Demokrasia ni mahusiano baina ya watu wakubwa kwa wadogo, tajiri kwa maskini.

Demokrasia hujumlisha na kurutubishwa na mila na desturi. Demokrasia halisi katika mtazamo huu ni ile inayofungua mianya mingi ya ushiriki wa umma katika harakati za kujiendeleza. Kwa hiyo demokrasia, katika tafsiri hii, haiwezi ikawa ni kitu cha kupatikana papo kwa papo. Ni mwenendo wa kudumu unaokua na kupanuliwa kila kukicha, na kwa maana hiyo demokrasia ili iwe endelevu ni lazima ijengeke katika misingi ya historia na utamaduni wa nchi. Haiwezi ikapandikizwa toka nje bali iruhusiwe kuchipua na kuota mizizi ndani ya jamii lakini bila kufumbia macho wala kuziba masikio kwa yale yanayotendeka mahali pengine. Ushauri ni kujifunza kutoka kwa wenzetu na wala si kuiga kikasuku. Misingi muhimu ya demokrasia haitofautiani kutoka nchi moja hadi nyingine. Lakini utekelezaji wake lazima uzingatie mazingira na hali halisi ya nchi husika.

Tukumbuke pia kuwa demokrasia haiishii kwenye uhusiano baina ya dola na wananchi tu. Demokrasia vilevile ni majumuisho ya mahusiano ndani ya jamii. Katika sura hii ya pili demokrasia huhitaji kuzingatia kwa dhati na kuweka mbele maadili ya kuvumiliana na

kutumia majadiliano kwa lengo la kupata muafaka. Katika mazingira ya siasa za ushindani ni vema tukajitahidi kuzielewa hoja na hisia za wale tunaoshindana, kwani bila wao kuwapo, utaratibu wa ushindani wa kisiasa inayorutubisha demokrasia hautanoga. **Upinzani si usaliti** na wala haistaili kuwa chanzo cha chuki katika jamii. Popote pale tulipo, iwe ni katika chama tawala au katika vyama vya upinzani **tunaitumia haki yetu ya kikatiba**. Aidha kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kisiasa na kijamii **tunatekeleza wajibu wetu wa kizalendo.** Sote sisi ni watanzania na ni imani yangu kwamba sote tuna uchungu wa Taifa letu.

Nina matumaini tutajipa fursa ya kutosha kutafakari kwa undani mafanikio tuliyoyapata na vilevile kuainisha maeneo yale ambayo bado yanahitaji kuboreshwa ili kuimarisha mfumo wetu wa siasa wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.Kwa mfano tunaweza kuanza kwa kila chama kuangalia ni jinsi gani chenyewe kinaweza kuchangia kufanikisha lengo hili la jamii kwa chama chenyewe kuimarisha demokrasia ndani ya chama husika.

Chama ambacho hakitilii maanani suala la umuhimu wa kujenga demokrasia ndani ya chama kwa kujiwekea kanuni zinazowezesha mjadala katika vikao kuendeshwa kwa kuvumiliana na kutofautiana kwa hoja bila kutukanana wala kudhalilishana wenyewe, kwa wenyewe hakiwezi kuienzi dhana ya uvumilivu wa kisiasa pindi kinakabiliwa na hoja za upinzani.Badala ya kutegemea nguvu ya hoja kukabili hoja ya upinzani kitajielekeza kuchochea jazba na hoja ya nguvu.

Uvumilivu wa kisiasa ni muhimu si tu baina ya vyama vyenye kutufatiana katika itikadi na sera bali hata ndani ya kila chama. Na mavuno yake kwa jamii ni makubwa, ikiwa kila mwanachama wa chama cha siasa atakuwa amelelewa katika maadili ya kuvumiliana na kuheshimiana. Mwanachama huyo atajenga mazoea ya kuheshimu na kuongozwa na katiba ya chama chake. Kwa maana hiyo chama kinakuwa ni chuo kinachowapatia mafunzo ya uraia na umuhimu wa kutii sheria na hususan, katiba ya nchi. Ikiwa shughuli za kisiasa zitaongozwa kwa kuzingatia katiba na sheria zilizowekwa ili

kuratibu shughuli za vyama vya siasa tutakuwa tumejiwekea msingi mzuri wa kujenga utamaduni wa kuvumiliana kisiasa.

Mambo yote haya yanaweza yakaonekana kuwa dhahiri mno kiasi hata cha kutufanya tuamini kuwa hayana mgogoro katika kuyatekeleza. Lakini kwa wale ambao wamepata fursa ya kuongoza vikao, watakiri kuwa mambo haya si rahisi kiasi hicho. Ni kweli chama ni taasisi, na kama taasisi, kuna muundo wa uongozi, kanuni na taratibu zilizo wazi kwa wanachama. Lakini vilevile haifai kupuuza ukweli kwamba chama ni wanachama. Katika sura hii ya chama kuwa ni wanachama ndipo ambapo hujitokeza matatizo. Wanachama ni binadamu, kila mmoja ana hisia na matarajio yake. Katika yote hayo upo uwezekano wa kuwepo mgongano katika matarajio binafsi ya wanachama na matarajio ya chama au jamii.Ingawa sio rahisi kuikana nafsi, ubinafsi ukiwekwa mbele zaidi ya matakwa ya jamii unaweza ukahatarisha umoja na mshikamano ndani ya jamii na taasisi.

Sababu hiyo hiyo ya kutanguliza ubinafsi inaweza kupelekea tushindwe kuona mantiki au uzito wa hoja inayotolewa na watu wengine na hasa wale tunatofautiana kisiasa. Badala yake hujiandaa kuzibomoa hoja hata kabla hatujazisikiliza na kuzitafakari kwa makini ili mradi zimetolewa na upande tunaoshindana nao.

Mtazamo wa namna hii siyo sahihi kwa chama wala jamii. Kupinga tu kwa ajili ya kupinga hakumjengi anayepinga. Badala yake humfanya aonekane kuwa asiyejua kupambanua mambo. Hii ni kweli kwa mtu binafsi na kwa chama vilevile . Ni kweli kazi ya chama cha upinzani ni kuzikosoa sera za chama tawala na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya serikali. Bila kufanya hivyo kitashindwa kuwapatia wananchi fursa ya kulinganisha sera ili hatimaye wafanye uamuzi wa busara. Lakini kazi hiyo lazima ifanywe kwa makini na uangalifu mkubwa kikipendekeza nini kinakusudia kufanya kikipewa ridhaa ya kuwa chama tawala. Vivyo hivyo kwa chama kilichoko madarakani. Haifai kulikataa jambo ilimradi limewasilishwa na upinzani. Mkabala huu ukigeuzwa kuwa mkakati wa kudumu wa chama tawala unaweza ukakidhoofisha chama hicho na kukipunguzia

hadhi. Lazima kionekane kuwa ni chemchem ya mawazo na mikakati mipya ili kiendelee kujijengea uhalali wa kuongoza jamii.

Mustakabali wa jamii ndio pekee unastahili kuwa kiungo baina ya wanachama wa vyama vyote. Pamoja na tofauti zetu za kisiasa tunayo mengi yanayo tuunganisha kama Watanzania na kwa pamoja tunawajibu wa kuijenga Tanzania. Sote tunatamani kuwarithisha watoto wetu Tanzania yenye amani na mshikamano, nchi ambamo kila mtu bila kubaguliwa ana fursa ya kujiendeleza. Tofauti za kisiasa hazinabudi kuwa chemchemi ya mawazo na mikakati ya kuongeza kasi ya maendeleo ya wananchi wetu.

Suala la Utawala Bora, kutekeleza kikamilifu misingi ya kidemokrasia, kuheshimu haki za binadamu, kupambana na kikamilifu na kero ya rushwa na kuleta maisha bora ka wananchi wetu, ni masuala ya kitaifa. Mambo haya yanahusu Vyama vyetu vyote vya siasa. Pia yanahusu Taasisi, Mashirika na Taasisi zetu mbali mbali. Vivyo hivyo masuala ya kujiwekea miiko kuhusu mambo ambayo yasifanyiwe mzaha. Haya ni pamoja na: Umoja na mshikamano wa

kitaifa, kudumisha utulivu na amani, kupambana na ubaguzi wa aina yoyote ile ikiwa ni wa misingi ya kikabila, dini, rangi au mtu atokako. Haya ni mambo ambayo tunapaswa sote kuyasimamia kikamilifu yasiwe ni mambo ambayo yanategemea ushabiki wa kichama. Kwa lugha nyingine Vyama vyetu vyetu vyote vya kisiasa viwe vinakubaliana kuhusu maadili haya.

Tukifanya hivyo tutaendelea kufanikiwa kujenga uchumi ambao pamoja na kuwa na majukumu ya kiserikali, lakini pia unatilia mkazo upasao kwa sekta binafsi, kuimarisha uzalishaji na kupeleka mbele gurudumu la maendeleo. Hakuna sababu kwa nini nchi yetu isifaulu katika kuboresha maisha ya watu wetu na kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa miongoni mwa nchi za mstari mbele katika vuguvugu la kuondokana na ufukara na umasikini na kusimama kidete kubadilisha mazingira duni ya uhusiano wa uchumi wa kimataifa.

Tanzania imebahatika kuwa mojawapo ya nchi za Afrika ambayo inasifika kuwa na Amani na Utulivu. Ni muhimu kudumisha

hali hii na kwa hiyo kudumisha sifa ya nchi yetu na kuimarisha mafanikio yake. Lakini pia ni muhimu kutambua kuwa hali hii haikua hivi hivi tu au kwa miujiza fulani. Ni rahisi kusahau kuwa Amani na Utulivu hujengwa. Ndio maana tuna deni kubwa kwa waasisi wa Taifa letu waliojenga misingi na nguzo imara ambazo ndizo zinategemeza amani na mshikamano ndani ya nchi yetu. Vile vile tunawajibika kuwarithisha watoto wetu, wajukuu, vitukuu na virembwe tunu hii tuliyoachiwa na wazee wetu.

Mchango wa waasisi wa taifa letu katika kujenga hisia nzito za utaifa, umoja na uzalendo wa kima cha juu hauwezi kusahaulika. Wahenga walinena na Marehemu Mwalimu Nyerere hakuchoka kutukumbusha kuwa **"ukiona vinaelea vimeundwa".** Tusisahau tamko lake kwa ulimwengu kuwa tunataka kuwasha mwenge kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro ili uangaze hata nje ya mipaka ya nchi yetu ukileta matumaini palipo na kukata tamaa, heshima na upendo palipojaa dharau.

Tuna haki ya kujivunia na kuienzi misingi thabiti iliyowekwa na kuimarishwa na waasisi wa Taifa letu ambao kwa kauli na vitendo walifanikiwa kulijengea heshima Taifa letu. Kuwaenzi ni kuendeleza yale mema waliotuachia.

Hapa ningependa kusisitiza kwamba katika mazingira halisi tunayokabiliana nayo ndani ya Bara letu inatupasa tukumbuke kwamba moja ya mambo ambayo husaidia sana kuwepo amani na utulivu ni kuwepo na demokrasia. Hapo hapo uzoefu umeonyesha kwamba demokrasia yenyewe hutegemea kuwepo kwa hali ya amani. Kwa hiyo ni mantiki isiyotetereka kwamba ni muhimu kwa wanademokrasia wote kwa pamoja kuwa watetezi wa kweli wa misingi ya demokrasia na haki za binadamu ambazo zikikiukwa husababisha madhara makubwa katika taifa.

Sote iwe ni katika vyama vyetu vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyama vya wafanyakazi, taasisi za dini na taasisi nyinginezo tunawajibika kuhakikisha kwamba katika maeneo yetu vitendo na mikakati yetu izingatie mambo haya ya msingi kwa mstakabali wa

taifa letu. Tusikubali kuyumbishwa katika mambo ya msingi. Wakati tunasherekea miaka 10 ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi katika nchi yetu, ni vyema tukakumbushana haya.

**Waheshimiwa Washiriki wa Kongamano,**

Tumo katika kipindi cha mageuzi ndani ya nchi yetu na katika Bara la Afrika na pia katika ulimwengu kwa jumla. Changamoto kubwa inayotukabili ni jinsi gani tutaweza kukitumia kipindi hiki, mabadiliko gani tutayafanya na kwa kiasi gani ili kuboresha hali za watu wetu na kuweza kupambana na changamoto na matatizo ya dunia ya utandawazi.

Nawashukuru kwa kunisikiliza na hivi sasa naomba kutamka kwamba Kongamano hili limefunguliwa rasmi.

**Asanteni.**